

# Shule Ya Biblia Ulimwenguni Kwa Njia Ya Kideo

Ilianza 1986



# UINJILISTI WA MTU BINAFSI

Mafunzo haya yametengenezwa ili ya saidie wanafunzi Shule ya Ulimwengu kwa njia ya ya kideo wasiotafuta kutunukiwa, wanaosomea nyumbani kwa kupata cheti. Mwanafunzi atatakiwa kuweka bidii katika mtaala mzima. Mwanafunzi asiyetaka kutunukiwa anaweza asijali kufuata mtaala na kutumia mafunzi apendavyo kwa manufaa yake ya kiroho.



*Shule Ya Biblia Ulimwenguni Kwa Njia Ya Kideo*
*130 Lantana Lane*
*Maxwell, Texas 78656-4231*
*Marekani.*

biblestudy@wvbs.org
http://www.wvbs.org/

*Shule Ya Biblia Ya Arusha*
*Sanduku la Barua 12163 Arusha*

*Tanzania.*

**Uinjilisti wa Mtu binafsi**
**Mtaala**

**I. HABARI KAMILI.**

- **A. Mkufunzi: Francis Wechesa**
- **B. Kozi hii kuna masomo 11**
- **C. Kila darasa litachukuwa dakika 45**

**II. MAELEZO NA KUSUDI**

- **A. Katika kozi hii tutajifunza kwa undani utaratibu katika uinjilisti hasa tukikazia utendaji.**
- **B. Masomo yatakayofundishwa yatahusu changamoto, matayarisho, kuepukana na vizuizi.**
- **C. Wanafunzi watajifunza namna ya kutumia lugha ya kushawishi.**
- **D. Wanafunzi watakuwa na uwezo bora wa kueleze injili katika mioyo ya watu waaminifu.**

**YATAKIWAYO DARASANI**

- **A. Utatakiwa kukariri madondoa yote.**
- **B. Leta insha ya muhula**

**MADONDOA**

- **A. Utatakiwa kuandika madondoa kila tunapoanza darasa.**
- **B. Uinjilisti wa mtu binafsi (1) mistari ya kukariri:**

**Mathayo 28:18-20 , Mark 16:15-16**
**Mdo. 8:4 , Warumi 1:15-16**
**Warumi 3:23 Warumi 6:23**
**Warumi 6:17 Warumi 10:14**

**INSHA YA MUHULA**

**Chagua aina kumi ya ubishi watu wanaoutumia kupinga umuhimu wa ubatizo kwa ondoleo la dhambi. Onyesha kutokana na Biblia kwa nini ubishi huo ni makosa. Insha iwe na kurasa kumi. Iwe tayari mwisho wa muhula.**

## UINJILISTI WA MTU BINAFSI
## UTANGULIZI.

**1. Hakuna mtu aliyezaliwa akiwa mwokoaji wa roho:**

**a.. Tunasoma kuhusu kufa kwa makanika, lakini sio kuzaliwa kwa makanika**

**b. Tunasikia Rais amekufa lakini hatusikii rais amezaliwa.**

**c. Tunasikia Mwinjilisti amefariki lakini hatusikii mwinjilisti amezaliwa.**

**d. Hatimisho: Makanika, Rais, Wainjilisti, hufanywa siyo huzaliwa.**

**2. Tunajifunza kufanya kwa kufanya:**

**a. Kusoma kitabu kuhusu kurusha ndege hakumfanyi mtu kuwa mrusha ndege.**

**b. Kusoma kitabu kuhusu kushana nguo, hakumfanyi mtu kuwa fundi cherehani.**

**c. Kusoma kitabu kuhusu kilimo hakumfanyi mtu bila shaka kuwa mkulima.**

**d. Kunatakiwa kuwa na mazoezi kuhusiana na vitu vile anavyojifunza.**

**e. Ndivyo inavyo kuhusu uinjilisti wa mtu binafsi.**

3. Kichocheo cha kuwafikia waliopotea:
   a) Waliopotea wameangamia katika jehenam ya milele.

   b) Injili ndiyo njia ya pekee ya kuwafanya watu

      kuokolewa.

   c) Tumekabidhiwa kuwahubiri watu injili
   d) Tunapaswa kuwajali waliopotea kama vile Kristo na Mungu walivyo wajali. (Lk. 19:10)
   e) Tunapaswa kuwa watumwa waaminifu.
   f) Ikiwa Mungu angeliwajali waliopotea kiasi wewe unavyowajali, wangapi wangelikuwa wameokoka?

4. Kuokoa roho zilizopotea ni matokeo katika mtu yule anayekaa ndani ya Kristo.
   a. Tutakuwa waokoaji wa roho zilizopotea siyo kwa sababu ya **kile tunacho kijua**, bali ni kwa sababu ya **yule tunayemjua**.

   b. Uinjilisti siyo kile tunachokifanya, bali ni kile mtu alaivyo.

5. Mtu anaanzaje kuwa mwinjilisti?

   a) Sali
   b) Jifunze.
   c) Fanya mazoezi
   d) Mtumainie Mungu.

   e) Kusanya makataba nzuri ya vitabu mbalimbali.

6. Kwa nini watu wengine huogopa kushirikiana na watu wengine imani yao?
   a) Wengine wanahofu kwamba, wataharibu badala ya kutengeneza.
   b) Wengine wanaogopa kushindwa.
   c) Wengine wanaogopa kwa sababu watakataliwa.
   d) Wengine hawajui la kusema.
   e) Wengine hawajui namna ya kuelezea injili.
   f) Wengine wanajisikia kwamba siyo karama yao.
   g) Wengine hawajui namna ya kuanza.
   h) Wengine hawajui namna ya kumalizia
   i) Wengine hawajisikii kama ni wajibu wao kufanya hivyo.

## MATENDO YA KUTANGULIA

1. Pata Biblia

**2.** Weka alama

**3.** Soma Biblia yako kila siku.

**4.** Panga muda wako kufanya kazi.

**5.** Omba ili Mungu

   a. akuongoze
   c. akupe hekima

**6.** Vaa vizuri
**7.** Kuwa msafi
**8.** Ni vizuri kuenenda wawili wawili ikiwezekana.
**9.** Lifahamu eneo lile vizuri. Ikiwezekana kuwa na ramani ya eneo husika.
**10.** Panga watu wakutembelea:
   a. Tangulia kuwaendea wale wenye matarajio mazuri.

b. Panga orodha ya watu unaowatarajia kutembelea katika eneo moja la mji kabla hujahamia kwingine. Hii itakusaidia kuokoa muda wako.

**11.** Kuwa na tract yenye jina la Kanisa juu yake ya kumwachia endapo utamkuta hayupo.

**12.** Usiuzibe mlango

**13.** U**<u>sianze</u>** mazungumzo ya Biblia ukiwa mlangoni.

a. Muda utakaouchukuwa mlangoni ni wakuingia ndani ya nyumba na kuanza mafunzo.

b. Hutaweza kuwaongoa tusipoweza kuwaomba wakae chini na kuanza kufunua Biblia pamoja nao.

**14.** Onyesha urafiki.

**15.** Kuwa na shauku, (moyo wa harara) Shauku huleta mafanikio.

**16.** Kuwa na adabu.

**17.** Fundisha kundi dogo. Usi ruhusu mwanafunzi wako kukupeleka mahali penye kundi kubwa.

**18.** Salamu za kushikana mikono ziwe zenye nguvu. Siyo goigoi.

**19.** Ukiwasalimia wakina mama usitie nguvu nyingi.

## MWENZA MKIMIA

1. Mwokoaji wa roho na mwenye dhambi wakae pamoja
2. Msaidie mwenye dhambi kufunua Biblia
3. Inamisha kichwa kwa i shara ya kukubali panapo stahili.
4. Kila mara unekana wakufurahia mafunzo.
5. Omba kimoyo moyo.
6. Ikihitajika angalia watoto kama wapo.
7. Kuwa kimya.

a. Isipokuwa tu kama mwenzako atakuomba kusema jambo.

b. Kama unaona kuna mahali panahitaji maelezo zaidi.

MJIO

1. Tumia sekunde kumi kama muda wa kujianda kuanza mafunzo.

2. Kunza Moyo Wa Kupenda. (KUMOWAKU)

3. Mjio wa maswali:

   a. Tumia mwaswali kukuza moyo wa kupenda

      1. “Je! Waliowengi watakwenda mbinguni?”
      2. “Je! Tuko chini ya amri kumi?”
      3. “Ikitokea ufe leo una uhakika wa kwenda mbinguni?”
      4. “Unajua chochote kuhusu kanisa la Kristo?

   b. Badaye tumia swali lingine kwa kuanzisha mafunzo: (Tumia swali #1 chini pamoja na #1 katika a. Hapo juu).

      1. “Ungependa kufahamu jinsi Biblia inavyosema kuhusu jambo hilo?”

      2. “Ungependa kufahamu Biblia inasema nini kuhsu jambo hilo?”

      3. “Ungependa kuwa na uhakika?”
      4. “Ungependa kufahamu?”

4. Shauku :

   a. Shauku huleta mafanikio.

   b. Ikiwa unafurahia uhusiano wako na Yesu, unaweza kuwafanya wengine nao wamfurahie.

c. Na kama hufurahii uhusiano wako na Yesu, huwezi kuwafanya wengine wafurahie.

d. Shauku huambukiza.

5. Usiwape vingi.

   a. Habari nyingi kwa  haraka hufanya watu kukata tamaa.
   b. Mpe mwanafunzi wako habari ya kutosha kuanzisha mafunzo tu.

6. Mambo mawili muhimu unayotakiwa kukumbuka katika mjio wako, ni kukuza moyo wa kupenda.

   a. Kuza moyo wa kupenda (KUMOWAKU)
   b. Patana siku ya kukutana tena--Fanya Miad(F.M)

MJIO WA MLANGONI

1. Onyesha urafiki. Unafuraha na unacho kitu cha ajabu cha kushirikiana naye.

2. Tafuta kitu kimoja cha kumsifia.

   a. Nyumba

   b. Bustani

   c. Mazingira

3. Mazunguzo:

   a. Je!  Kuna mtu ambaye amekuletea kikaratasi kama hiki?
   b. Ni vema ni pitia hapa, sema ukiwa na shauku.
   c. Ebu na ni kuambie tunachokifanya:

1. Kwanza nitaanza kukuambia kile ambacho hatufanyi:
    a. Hatutafuti mchango.
    b. Hatujaribu kuuza vitabu vyetu.

2. Haya ndiyo tunayoyafanya:
    a. Tunafanya hudumu kwa jamii.
    b. Tunajaribu kurudisha taifa hili kwa Mungu, na ninaamini hayo ndiyo yanayotakiwa. Unaonaje? Subiria jibu.
    c. Ni naamini kwamba sote tunatakiwa kurudia Biblia na kuanza kuishi kwa kufuata misingi iliyomo ndani yake. Unaonaje? (subiria jibu)
    d. Unasoma sana Biblia? Bila kujali jibu lake wewe endelea tu.
    e. Tunatembelea wakazi wa eneo hili lote.
    f. Tunatoa huduma ya kugawa tract hizi bure na kuwasajili watu kuanza kusoma neno la Mungu wakiwa nyumbani mwao.
        1. Haina masharti yoyote.
        2. Hafungamani na Madhehebu yo yote.
        3. Tayari tumekuwa tukijifunza majirani zako na wameshukuru sana.

d. Sasa ningelipenda iwe rahisi kwako sana iwezekanavyo.
    1. Tunaweza tukaingia na kujifunza kama unapenda.
    2. Au kama hawezekani turudi siku nyingine. (Taja siku unayoipendekeza.)
    3. Ni siku gani inaweza ikawa nzuri kwako?

# MJIO WA MLANGONI (2)

Mijio hii miwili imependekezwa na John Kimbrough

John alisema, mjio huu unakuingiza katika kila aina ya mlango:

Habari za asubuhi/mchana/jioni. Sisi ni jirani zako. Jina langu ni **John Kimbrough**, na huyu ni **James Smith.**
Tulifikiria ingelizunguka asubuhi/mcha /jioni hii na kuwaelezea majirani zetu kuhusu huduma ya bure kwa jamii inayotolewa na pengine hujajua. Je! Unayonafasi tuingie?

Huduma ya bure hii ilikuwa ni kutoa ushauri, madarasa ya biblia kwa watu wa rika zote, masomo ya korespondesi (kwa njia ya posta). Na mafundisho ya biblia ya bure manyumbani. Jaribu kuomba kujifunza nao mafundisho ya biblia bure nyumbani wakati huo.
Huu ni mjio alioupendekeza John Kimbrough kuwatafuta walionahamu:
Habari gani? Jina langu ni John Kimbrough na huu ni rafiki yangu James Smith. Tumetoka leo hii kuwambia jirani zetu huduma hii ya bure inayotolewa na kanisa la Kristo; kama ushauri, madarasa ya Biblia kwa rika zote, mafunzo ya korespondesi (njia ya posta). Unashikamana na kanisa lolote katika eneo hili? Kama hana kanisa unaweza kumwomba kumwelezea kuhusu kanisa, kama anayo, uliza kama anajifunza biblia nyumbani mwake? Akisema ndiyo, sema, vema sana, ninajua utafurahia mafunzo mafupi haya.
Ni naweza ni kaingia? Ukimwona kama anasita, uliza kama anaweza kukuruhusu kumwuliza swali, “kama ungelikufa leo hii, unajua kwa uhakika kwamba ungelikwenda mbinguni?” Kama jibu ni ndiyo uliza kama anaweza kushirikiana na wewe katika hilo. Akikubali kukuelezea, msikilize kwa makini ukiandika kila anacho kisema. Uliza ulikujaje kujua kwamba ukifa leo utakwenda mbinguni.

# Uinjilisti Binafsi

4th July 2002

| No. | Name | Mtihani | Madondoa(8) | Insha | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashers Mbasha | 96 | 38 | 50 | 61 |
| 2. | Devota | 68 | 59 | 71 | 62 |
| 3. | Magilani Kiraho | 100 | 36 | 35 | 57 |
| 4. | Laurian Munishi | 71 | 64 | 91 | 73 |
| 5. | Max Danieli | 79 | 48 | 30 | 52 |
| 6. | Margaret Wechesa | 100 | 90 | - | |
| 7. | Wilson Maturo | 28 | 37 | - | 22 |
| 8. | Anna Minja | 78 | 37 | - | 38 |
| 9. | Fiofilo Mukota | 96 | 73 | - | 56 |
| 10. | Marigareta Augustino | 82 | | | |